# Mabadiliko ya Kifonolojia ya Istilahi za Kiingereza katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani kutoka Covid 19

*Editha Adolph*
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere*

**Ikisiri**

**Miongoni mwa mambo yanayozifanya lugha kukopa na kutohoa istilahi ni mlipuko wa magonjwa. Gonjwa la COVID 19 limekuwa sababu ya lugha ya Kiswahili ama kukopa, kutohoa au kuhuisha istilahi za Kiingereza. Makala haya yanachunguza mabadiliko ya kifonolojia ya istilahi za Kiingereza katika Kiswahili kwa kujikita katika istilahi zinazohusiana na COVID 19. Katika kuchunguza mabadiliko ya kifonolojia ya utohozi wa istilahi hizo tumeongozwa na nadharia ya NFZ (Nadharia ya Fonolojia Zalishi) iliyoasisiwa na Noam Chomsky na Morris Halle (1968). Nadharia hii ni muafaka katika makala haya kwani inatoa mwongozo katika kuchunguza na kuchanganua mabadiliko ya sauti yanayojitokeza baada ya istilahi kutoholewa kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Makala haya yanashughulikia mojawapo ya matokeo ya utohozi unaohusisha lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Ili kufikia malengo ya makala yetu, zimetumika mbinu za hojaji na uchambuzi wa matini. Mbinu ya hojaji hurahisisha ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda mfupi (Mugenda na Mugenda 2003). Mbinu ya kuchambua matini imejumuisha usomaji wa nyaraka za kitaaluma kwa minajili ya kupata data ya makala yetu.**

**Maneno Muhimu:** *COVID 19*, Huhisha, Fukiza, *Lockdown, Corona, Mask* & *Quarantine*

**Utangulizi**

Zipo sababu mbalimbali za utohozi wa istilahi za LC katika LP. Miongoni mwa sababu hizo ni maendeleo ya sayansi na teknolojia, shughuli za kiuchumi, ukoloni, muwasala kati ya wazungumzaji wa lugha moja na nyingine na sababu nyingine kadha wa kadha, (Akida 2008; Shembilu 2010; Adolph 2019). Mbali na sababu hizo, ni dhahili kuwa mlipuko wa magonjwa ni miongoni mwa sababu za utohozi wa istilahi za LC katika LP. Mnamo Disemba 2019, kulizuka ugonjwa ujulikanao kama COVID 19 uliosababishwa na kirusi cha korona. Ugonjwa huu ulianzia mataifa ya Ulaya na China na kuenea kwa kasi ulimwenguni kote 2020. Kutokana na kasi hiyo ugonjwa huu umeenea ulimwenguni kote na kusababisha vifo vingi vya watu. Kwa vile ugonjwa huu umetapakaa ulimwenguni kote, lugha mbalimbali

zimejipatia istilahi mpya ama kwa kuzitohoa au kuzikopa kama zilivyo kutoka katika lugha ya Kiingereza na lugha za Kibantu.[1]

Ikumbukwe kuwa si istilahi zote ni mpya, la hasha, kuna baadhi ya istilahi ni mpya kabisa na nyingine zimehuishwa. Tunaposema zimehuishwa tuna maana kuwa zilikuwepo na hazikutumika sana isipokuwa zimeshika kasi katika kipindi hiki cha mlipuko wa Korona. Makala haya yanaangazia utohozi wa istilahi hizo kutoka lugha ya Kiingereza katika Kiswahili. Kwa mujibu wa data ya makala haya istilahi mpya ni moja tu, yaani COVID 19 na istilahi nyingine zimehuishwa.

**Istilahi Mpya na Zilizohuishwa**

Kama tulivyotangulia kudadavua hapo juu, ni kwamba siyo istilahi zote zinazoshughulikiwa katika makala haya ni mpya. Istilahi nyingi zilikuwepo kabla isipokuwa zimehuishwa na kushika kasi wakati huu wa mlipuko wa ugonjwa huu wa COVID 19. Jedwali hapa chini linaweka wazi suala hilo:

**Jedwali 1: Istilahi Mpya za Korona na zile Zilizohuishwa Kutokana na Kirusi cha Korona**

| Istilahi za Kiingereza | Istilahi za Kiswahili | Matamshi | Aina ya Istilahi | Maana ya Istilahi |
|---|---|---|---|---|
| Case | *Kesi* | /keɪs/ | Imehuishwa | Idadi ama ya vifo au wagonjwa. |
| Corona | *Korona* | /kə'roʊnə/ | Imehuishwa | Aina ya virusi vinavyosababisha maradhi kwa wanyama na binadamu, jamii kadhaa za virusi vya korona vinafahamika kusababisha madhara na maambukizi kwenye njia ya hewa na mfumo wa upumuaji. |

[1] Istilahi nyingi zilizokopwa au kutoholewa kutoka lugha za Kibantu ni zile zilizohusiana na tiba. Kwa mfano, mitishamba ya kujifukiza na kunywa. Hii ni kutokana na jitihada nyingi zinazofanywa na binadamu katika suala zima la kujikinga na janga la kirusi cha Korona.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| COVID 19 | *Kovidi 19* | /kəvɪdɪ ˌnaɪn'tiːn/ | Mpya | Maradhi yasababishwayo na virusi vya korona. |
| Lockdown | *lockdown* | /lɑːk daʊn/ | Imehuishwa | Tendo la kukaa nyumbani pasipo kwenda popote mathalani, kazini, kwenye shughuli za kiuchumi, michezoni, masomoni n.k |
| Mask | *maski* | /mæsk/ | Imehuishwa | Vazi linalovaliwa usoni na mtu yeyote agh. kumkinga dhidi ya upepo, harufu mbaya au vijidudu vya magonjwa kwenye sehemu za macho pua na mdomo. |
| Pandemic | *pandemiki* | /pæn'demɪk/ | Imehuishwa | Ueneaji wa magonjwa ya kuambukiza katika eneo kubwa, kwa mfano, bara au hata dunia nzima. |
| Quarantine | *karantini* | /'kwɔːrəntiːn/ | Imehuishwa | Muda maalumu wa kuwafungia watu/wanyama ama wanaoshukiwa au wana ugonjwa fulani kwa lengo la kuzuia ueneaji wa ugonjwa huo. |
| Sanitizer | *sanitaiza* | /sænɪtaɪ'zeɪ/ | Imehuishwa | Kimiminika cha kujitakasia kwa lengo la kuua bakteria. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Ventilator | *ventileita* | /'ventɪleɪtər/ | Imehuishwa | 1. Kifaa kinachosaidia kuingiza hewa katika eneo lililofungwa.<br>2. Mashine inayomsaidia binadamu kupumua vema kwa kuruhusu hewa iingie na kutoka kwenye mapafu. |
| Virus | *kirusi* | /'vaɪrəs/ | Imehuishwa | Kiumbe kidogo sana kisababishacho magonjwa kwa binadamu, wanyama na hata mimea. |

**Chanzo:** Data ya Uwandani na Maktabani, 2020

**Mabadiliko ya Kifonolojia**

Suala la utohozi huhusisha mabadiliko kadhaa ya kifonolojia. Miongoni mwa mabadiliko mengi ya kifonolojia, makala haya yanashughulikia udondoshaji, uchopekaji pamoja na usahilishaji wa irabu unganifu na irabu ndefu kuwa irabu sahili tu. Habibu (2013) anatoa ufafanuzi juu ya mabadiliko ya kifonolojia kwa kusema kuwa: mabadiliko ya kifonolojia ni moja kati ya vipengele vya taaluma ya isimu. Katika mabadiliko haya kinachozingatiwa ni mabadiliko yanayoweza kutokea wakati sauti zinapofuatana.

**Udondoshaji**

Udondoshaji hutokea pale ambapo irabu au konsonanti ya LP huondolewa katika istilahi iliyotoholewa kutoka LC (Adolph, 2019). Katika mchakato huu sauti iliyokuwepo awali katika istilahi husika hudondoshwa kutokana na mfuatano wake na sauti nyingine kutokubalika katika mfumo wa lugha inayohusika. Udondoshaji hufanyika ili kuzifanya istilahi za Kiingereza ziendane na matamshi ya istilahi za Kiswahili (Adolph, 2014). Baadhi ya istilahi katika Jedwali Na. 1 ni vigumu kutamkika katika Kiswahili hadi baadhi ya konsonanti zidondoshwe:

**Jedwali Na. 2: Udondoshaji**

| Istilahi za Kiingereza | Istilahi za Kiswahili | Matamshi | Maana ya Istilahi |
|---|---|---|---|
| Case | *kesi* | /keɪs/ | Idadi ama ya vifo au wagonjwa. |
| Corona | *korona* | /kə'roʊnə/ | Aina ya virusi vinavyosababisha maradhi kwa wanyama na binadamu, jamii kadhaa za virusi vya korona vinavyosababisha madhara na maambukizi kwenye njia ya hewa na mfumo wa upumuaji. |
| Quarantine | *karantini* | /'kwɔːrəntiːn/ | Muda maalumu wa kuwafungia watu/wanyama ama wanaoshukiwa au wana ugonjwa fulani kwa lengo la kuzuia ueneaji wa ugonjwa huo. |
| Sanitizer | *sanitaiza* | /sænɪtaɪ'zeɪ/ | Kimiminika cha kujitakasia kwa lengo la kuua bakteria. |
| Ventilator | *ventileita* | /'ventɪleɪtər/ | 1. Kifaa kinachosaidia kuingiza hewa katika eneo lililofungwa. 2. Mashine inayomsaidia binadamu kupumua vema kwa kuruhusu hewa iingie na kutoka kwenye mapafu. |

**Chanzo**: Data ya Uwandani na Maktabani, 2020

Jedwali hili linaonesha bayana kuwa baadhi ya sauti hudondoshwa wakati wa utohozi wa istilahi. Data inaonesha kuwa miongoni mwa sauti zilizodondoshwa ni /ɪ/ katika istilahi */keɪs/*, na */sænɪtaɪ'zeɪ/* zilizotoholewa kutoka Kiingereza kuja Kiswahili. Baada ya udondoshaji huo, zimepatikana istilahi za Kiswahili *kesi* na *sanitaiza*. Aidha, sauti /ʊ/ imedondoshwa katika istilahi ya Kiingereza */kə'roʊnə/* na kutupatia istilahi ya Kiswahili *korona*. Sauti /w/ imedondoshwa katika istilahi */'kwɔːrəntiːn/* na kutupatia istilahi ya Kiswahili *karantini*. Halikadhalika, sauti /r/ katika istilahi ya Kiingereza */'ventɪleɪtər/* imedondoshwa na baada ya udondoshwaji wa sauti hiyo tumepata istilahi ya Kiswahili *ventileita*.

Shembilu (2010) anasema kuwa, “Katika Kiarabu, konsonanti pacha ni jambo la kawaida sana lakini si katika Kiswahili. Likitokea neno lina tabia kama hiyo na likatoholewa katika Kiswahili ni lazima konsonanti moja idondoshwe”. Kutokana na hoja hiyo tunaweza kusema kuwa istilahi zinazotoholewa katika Kiswahili ilhali zina mkururo wa konsonanti, konsonanti mojawapo hizo hudondoshwa isipokuwa istilahi chache zinazoghairi mchakato huu hubaki vilevile.

Naye Massamba (2007) anaeleza kuwa mchakato wa udondoshaji unahusu kuachwa kwa sauti fulani katika matamshi wakati mofimu mbili zinapokabiliana. Ni dhahiri kuwa mchakato wa udondoshaji hutokea katika mazingira ambayo sauti iliyokuwepo awali hutoweka. Kwa ujumla, utafiti huu umebaini kuwa utohozi wa istilahi zilizochunguzwa umeambatana na mabadiliko anuwai ya kifonolojia hususan mchakato wa udondoshaji.

Kwa mujibu wa data ya makala haya, inaonesha kuwa baadhi ya vitamkwa vya istilahi za COVID 19 za Kiingereza vimezingatia ruwaza maalum kwa kiasi kikubwa na kwa kiasi kidogo ruwaza maalumu haikuzingatiwa. Hali hii imejitokeza kutokana na sababu ya kutokuwa na kanuni moja inayotawala wakati wa udondoshaji. Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.1 hapo juu, data inaonesha kuwa miongoni mwa sauti zilizodondoshwa ni /ɪ/ katika istilahi */keɪs/*, na */sænɪtaɪ'zeɪ/* zilizotoholewa kutoka Kiingereza kuja Kiswahili. Sauti hii imedondoshwa baada ya kufuatana na irabu /e/ ya juu mbele. Hali hii haikujitokeza katika istilahi ya Kiingereza */'ventɪleɪtər/* kwani imetoholewa katika Kiswahili kama *ventileita.* Hapa tulitegemea sauti /i/ idondoshwe kwani imefuatana na sauti /e/ kama ilivyojitokeza kwa istilahi tajwa hapo juu. Hii ni kutokana na sababu tulizozitaja hapo awali.

Aidha, sauti /ʊ/ imedondoshwa katika istilahi ya Kiingereza */kə'roʊnə/* baada ya kuwa imefuatana na sauti /o/ na kutupatia istilahi ya Kiswahili *korona*. Lakini sauti hiyohiyo haikudondoshwa katika istilahi ya Kiingereza */la:k daʊn/* kwani imatoholewa kama *lockdown*[2] katika Kiswahili. Na badala yake imebadilika na kuwa sauti /w/ hii ni kutoka an sababu kuwa katika lugha ya Kiswahili maneno huandikwa vilevile kama yasikikavyo tofauti na lugha ya Kiingereza ambapo maandishi na matamshi hutofautiana. Halikadhalika, sauti /a/ katika istilahi ya Kiingereza */'vaɪrəs/* imedondoshwa baada ya kufuatana na sauti /i/. Jambo hili halikujitokeza katika istilahi ya Kiingereza */sænɪtaɪ'zeɪ/* tukapata istilahi ya Kiswahili *sanitaiza* ambapo tulitegemea idondoshwe kutokana na kufuatana na sauti /a/ kama ilivyojitokeza katika istilahi */'vaɪrəs/.* Sababu zimekwishaelezwa hapo juu.

Kwa ujumla, makala haya yamebaini kuwa utohozi wa istilahi zilizochunguzwa umeambatana na michakato anuwai ya kifonolojia hususan mchakato wa udondoshaji. Kanuni ya udondoshaji inafafanuliwa hapa chini:

Kanuni ya Udondoshaji:

/ɪ/ → /ø/ / -K
/ʊ/ → /ø/ / -K
/w/ → /ø/ / -I

[2] Istilahi hii ya Kiingereza imeingizwa katika Kiswahili kama ilivyo katika lugha ya Kiingereza isipokuwa kuna tofauti ndogo ya kimatamshi kati ya wazungumzaji wa Kiingereza na wale wa Kiswahili katika istilahi hii.

/ɪ/ ⟶ /ø/ I-
/r/ ⟶ /ø/ I-

**Ufafanuzi wa Kanuni**

Sauti /ɪ/ imedondoshwa katika istilahi za Kiingereza zilizotoholewa katika Kiswahili katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti. Sauti hiyohiyo pia imedondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na irabu. Aidha, sauti /ʊ/ imedondoshwa katika mazingira ya kufuatiwa na konsonanti. Sauti /w/ nayo imedondoshwa katika mazingira ya kufuatiwa na irabu. Halikadhalika sauti /r/ imedondoshwa katika mazingira ya kutanguliwa na irabu. Baada ya kufafanua mchakato wa udondoshaji tuangalie mchakato wa uchopekaji.

**Uchopekaji**

Huu ni mchakato wa kifonolojia unaofanyika kwa kuingiza kipashio, vipashio au sauti (irabu au konsonanti) katika istilahi iliyotoholewa kutoka LC na kubadili matamshi ya istilahi hiyo katika LP kwa lengo la kuyafanya matamshi hayo yaendane na ya LP. Makala haya yanaonesha jinsi ambavyo sauti za Kiingereza hutoholewa katika Kiswahili kwa kuchopekwa baadhi ya vitamkwa ili ziweze kukubalika katika mfumo wa lugha ya Kiswahili. Uchopekaji ni utaratibu wa kuingiza kipashio katika neno ambacho hakikuwepo awali (Eliah, 2012). Katika utafiti huu imebainika kuwa utohozi wa istilahi huambatana na matumizi ya mchakato wa uchopekaji. Madai haya, yanathibitishwa kwa mifano kadhaa iliyotolewa katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 2: Uchopekaji**

| Istilahi za Kiingereza | Istilahi za Kiswahili | Matamshi | Maana ya Istilahi |
|---|---|---|---|
| Case | *Kes**i*** | /keɪs/ | Idadi ama ya vifo au wagonjwa. |
| COVID 19 | *kovid**i** 19* | /kəvɪdɪ ˌnaɪn'tiːn/ | Maradhi yasababishwayo na virusi vya korona. |
| Mask | *mask**i*** | /mæsk/ | Vazi linalovaliwa usoni na mtu yeyote agh. kumkinga dhidi ya upepo, harufu mbaya au vijidudu vya magonjwa kwenye sehemu za macho pua na mdomo. |
| Pandemic | *pandemik**i*** | /pæn'demɪk/ | Ueneaji wa magonjwa ya kuambukiza katika eneo kubwa, kwa mfano, bara au hata dunia nzima. |
| Virus | *kirus**i*** | /'vaɪrəs/ | Kiumbe kidogo sana kisababishacho magonjwa kwa binadamu, wanyama na hata mimea. |

**Chanzo**: Data ya Uwandani na Maktabani, 2020

Jedwali hili linaonesha mifano mbalimbali ya istilahi zilizotoholewa kwa kutumia mchakato wa uchopekaji. Kwa mfano, irabu /*i*/ ya juu mbele imechopekwa katika istilahi za Kiingereza: */keɪs/, /kəvɪdɪ ˌnaɪn'tiːn/, /mæsk/, /pæn'demɪk/* na */'vaɪrəs/* Baada ya mchakato huu tumepata istilahi za Kiswahili: *kes**i***, *kovid**i** 19*, *mask**i***, *pandemik**i*** na *kirus**i***.

Kinyume na maelezo hayo, data inaonesha kuwa hakuna mabadiliko ya kifonolojia kwa baadhi ya istilahi za Kiingereza kwani hazikufanyiwa mabadiliko ya uchopekaji japokuwa istilahi husika zilikuwa na mkururo wa konsonanti. Suala hili limejitokeza katika istilahi kama vile: *maski*. Kutokufanyika kwa mchakato huu katika istilahi tajwa kumesababisha ujitokezaji wa muundo mpya wa silabi katika Kiswahili kama vile: KKI. Hivyo, mchakato huu haufuati ruwaza maalumu katika ufanyikaji wake.

Aidha, imeonekana kuwa istilahi zote za Kiingereza zinazoishia na konsonanti hufanyiwa mchakato wa uchopekaji mwisho. Kwa mfano, istilahi, */keɪs/*, */mæsk/*, */pæn'demɪk/* na */'vaɪrəs/* zimechopekwa irabu mwishoni na kutupatia istilahi za Kiswahili: *Kesi*, *maski*, *pandemiki*, na *kirusi*. Uchopekaji mwisho hasa kwenye istilahi zinazoishia na konsonanti unaonekana kutokuwa na ruwaza maalamu ya

kufanyiwa mabadiliko hayo kwani istilahi *COVIDI nineteen* na *Lockdown* hazijachopekwa irabu mwishoni.

Kanuni ya Uchopekaji

$$\left\{ \quad \right\} \theta \longrightarrow \; / \, /i/ \;\; /K\text{-}/$$

**Ufafanuzi wa Kanuni ya Uchopekaji**

Kanuni ya uchopekaji inaonesha kuwa irabu ya juu mbele /*i*/ imechopekwa kwenye istilahi: *kes**i***, *kovid**i** 19*, *mask**i***, *pandemik**i*** na *kirus**i***. Kama ilivyodokezwa hapo awali, uchopekaji umefanyika ili kuondoa mkururo wa konsonanti. Kwa ujumla, kutokana na data iliyopatikana uwandani, mtafiti anahitimisha kuwa istilahi hutoholewa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili kwa kuchopekwa irabu katikati ili ziweze kukubalika katika mfumo wa lugha ya Kiswahili.

**Usahilishaji wa Irabu Unganifu na Irabu Ndefu**

Usahilishaji wa irabu unganifu na irabu ndefu pia ni mchakato wa kifonolojia ufanyikao katika suala zima la utohozi. Katika mchakato huu irabu ndefu za Kiingereza hufupishwa na irabu unganifu za Kiingereza husahilishwa katika Kiswahili ili kupata irabu fupi na sahili kama zilivyo irabu za Kiswahili. Kiswahili kina irabu tano ambazo ni /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/ na /u/. Aidha, kuna tofauti kati ya mfumo wa irabu za Kiingereza na za Kiswahili. (Mgullu, 1999; Njogu, 2006; Mweri, 2010). Utohozi huzifanya irabu za Kiingereza kuingia katika mfumo wa irabu za Kiswahili. Ufuatao ni ufafanuzi wa tofauti ya irabu za Kiingereza na Kiswahili:

**Jedwali Na. 3: Irabu za Kiingereza na Kiswahili**

| Irabu Ndefu za Kiingereza | Mifano | Irabu Fupi za Kiingereza | Mifano | Irabu za Kiswahili | Mifano |
|---|---|---|---|---|---|
| /a:/ | /ə'da:ptər/ | /æ/ | /hæt/ | /a/ | Teknolojia |
| /e:/ | /'e:ɪ.gɑ:r e:ɪ.gɑ:r/ | /ə/ | /ə'baʊt/ | /ɛ/ | Jeti |
| /i:/ | /kli:əsʊt/ | /ʌ/ | /hʌt/ | /i/ | Injini |
| /o:/ | /ə'do:ʊbi/ | /ɛ/ | /bɛt/ | /ɔ/ | Lebo |
| /u:/ | /bu:t/ | /ɪ/ | /bɪt/ | /u/ | Globu |
| | | /ɔ/ | /bɔr/ | | |
| | | /ʊ/ | /pʊt/ | | |

**Chanzo**: Fromkin na Rodman (2003) na Utafiti wa Uwandani (2020)

Data ya utafiti huu inaonesha kuwa Kiingereza kina irabu sahili na irabu unganifu tofauti na lugha ya Kiswahili yenye irabu sahili pekee. Jumla ya irabu sahili za Kiingereza ni 12 (irabu ndefu 5 na fupi 7). Aidha, irabu unganifu katika

Kiingereza ziko za aina mbili: irabu unganifu zinazohusisha irabu mbili na zinazohusisha irabu tatu kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 4 hapa chini.

**Jedwali Na. 4: Irabu Unganifu za Kiingereza**

| Irabu unganifu Mbili | Mifano | Irabu unganifu Tatu | Mifano |
|---|---|---|---|
| /ai/ | /faɪtoʊ'ʤesis/ | /aʊə/ | /'paʊər/ |
| /oi/ | /soi/ | /aɪə/ | /'laɪər/ |
| /ɔɪ/ | /'ælɔɪ/ | /oʊə/ | /'loʊər/ |

**Chanzo**: Fromkin na Rodman (2003) na Utafiti wa Uwandani (2020)

Vielelezo hivi vya irabu za Kiswahili na Kiingereza vimetusaidia katika ulinganishaji wa irabu za lugha hizi hasa katika mabadiliko ya ufupishaji na usahilishaji wa irabu kama mifano inavyoonesha katika Jedwali Na. 5:

**Jedwali Na. 5: Usahilishaji wa Irabu Unganifu na Irabu ndefu**

| Istilahi za Kiingereza | Istilahi za Kiswahili | Matamshi | Maana ya Istilahi |
|---|---|---|---|
| Case | *Kesi* | /k**eɪ**s/[3] | Idadi ama ya vifo au wagonjwa. |
| Corona | *Corona* | /kə'r**oʊ**nə/ | Aina ya virusi vinavyosababisha maradhi kwa wanyama na binadamu, jamii kadhaa za virusi vya korona vinafahamika kusababisha madhara na maambukizi kwenye njia ya hewa na mfumo wa upumuaji. |
| COVID 19 | *kovidi nineteen* | /kəvɪdɪ ˌnaɪn'tiːn/ | Maradhi yasababishwayo na virusi vya korona. |
| Lockdown | *Lockdown* | /lɑːk d**aʊ**n/ | Tendo la kukaa nyumbani pasipo kwenda popote mathalani, kazini, kwenye shughuli za kiuchumi, michezoni, masomoni n.k |

[3] Istilahi moja inaweza kufanyiwa zaidi ya badiliko moja. Kwa mfano istilahi hii imefanyiwa mabadiliko ya udondoshaji na usahilishaji wa irabu unganifu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Virus | *Kirusi* | /'v**aɪ**rəs/ | Kiumbe kidogo sana kisababishacho magonjwa kwa binadamu, wanyama na hata mimea. |

**Chanzo**: Utafiti wa Uwandani (2020)

Katika Jedwali Na. 5 imebainishwa wazi jinsi irabu kadhaa zilivyofupishwa. Kwa mfano, katika istilahi ya Kiingereza: */l**ɑ**ːk d**aʊ**n/* irabu /ɑː/ imefupishwa tukapata istilahi ya Kiswahili: ***lo**ckdown*.[4] Vilevile, irabu /iː/ katika istilahi */kəvɪdɪ ˌnaɪn't**i**ːn/*, */'kwɔːrənt**i**ːn/* nayo sauti */ɔː/* katika istilahi */'kwɔːrəntiːn/* za Kiingereza imefupishwa tukapata istilahi ya Kiswahili: *kovidi 19* na *karantini*. Alama ː kama ilivyotumika katika istilahi mbalimbali inawakilisha sauti ndefu. Aidha, mifano katika Jedwali Na. 4.5 inaonesha wazi kuwa mchakato wa usahilishaji umezifanya irabu unganifu za Kiingereza kuwa irabu sahili katika Kiswahili. Kwa mfano, irabu unganifu katika istilahi za Kiingereza kama vile: */k**eɪ**s/*, */kə'r**oʊ**nə/* na */'v**aɪ**rəs/* zimesahilishwa katika Kiswahili na kutupatia istilahi: *kesi, korona* na *kirusi*.

Kwa mujibu wa data ya makala haya, imegundulika kuwa hakuna ruwaza maalumu iliyofuatwa katika madiliko ya kifonolojia ya usahilishaji wa irabu unganifu na irabu ndefu. Hii ni kutokana na sababu kuwa baadhi ya irabu unganifu zimesahilishwa na baadhi kuonekana kuwa vighairi. Kwa mfano, irabu zilizosahilishwa ni kama vile: /ei/ katika istilahi */keɪs/* ya Kiingereza na kuwa *kesi* katika Kiswahili, /oʊ/ katika istilahi ya Kiingereza */kə'roʊnə/* na kuwa *korona* katika Kiswahili, */aɪ/* katika istilahi ya Kiingereza */'vaɪrəs/* tukapata istilahi ya Kiswahili *kirusi*. Kinyume na mabadiliko hayo, sauti /aɪ/ katika istilahi ya Kiigereza */kəvɪdɪ ˌnaɪn'tiːn/* na sauti */ei/* katika istilahi */'ventɪleɪtər/* hazikusahilishwa na badala yake zimebaki kama zilivyo katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na kutofanyika kwa mabadiliko hayo, tumepata istilahi za Kiswahili: *COVID nineteen* na *ventileita*.

Kama ilivyo katika mabadiliko mingine, mchakato wa ufupishaji na usahilishaji wa irabu unaongozwa na kanuni kadhaa za kiisimu kama ilivyooneshwa katika kanuni ifuatayo:

Kanuni ya Ufupishaji wa Irabu:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| iː | → | i | / | /K-/ |
| ɔː | | ɔ | | /K-/ |
| ɑː | | ɑ | | /-K/ |
| ei | | e | | /K-K/ |

[4] Istilahi hii imefanyiwa mchakato wa uunganishaji wa irabu tu, bado inatamkwa na kuandikwa hivyohivyo katika Kiswahili kama ilivyo katika lugha ya Kiingereza. Haijafanyiwa marekebisho zaidi kama ilivyojitokeza katika istilahi nyinginezo. Kwa mfano, virus-kirusi.

**Ufafanuzi wa Kanuni**

Irabu ndefu /ɔ:/ imejitokeza kama irabu fupi /ɔ/. Vilevile, irabu ndefu /ɑ:/ imejitokeza kama irabu fupi /ɑ/. Halikadhalika, sauti /ei/ katika istilahi za Kiingereza zimesahilishwa na kujitokeza kama sauti /e/ katika Kiswahili. Sauti /ei/ katika istilahi za Kiingereza zimesahilishwa na kujitokeza kama sauti /a/ katika Kiswahili. Nazo Sauti /ai/ katika istilahi ya Kiingereza zimesahilishwa na kujitokeza kama sauti /i/ katika Kiswahili. Halikadhalika, Sauti /əʊ/ katika istilahi za Kiingereza zimesahilishwa na kuwa sauti /o/ katika Kiswahili.

**Hitimisho**

Makala haya yamechunguza utohozi wa istilahi za Kiingereza katika Kiswahili kwa kujikita katika istilahi za COVID 19. Utohozi uliochunguzwa ni ule uliohusisha mabadiliko ya kifonolojia. Mabadiliko hayo ni kama vile: udondoshaji, uchopekaji pamoja na usahilishaji wa irabu unganifu na irabu ndefu.

Kuna uwezekano wa kuwepo kwa mabadiliko mengi ya kifonolojia yanayohusiana na utohozi wa istilahi za COVID 19 kutoka lugha ya Kiingereza kuja Kiswahili ambayo hayajashughulikiwa katika makala haya. Hata hivyo, mtafiti wa makala haya amejiridhisha kuwa mabadiliko yaliyochunguzwa yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika suala zima la utohozi wa istilahi za COVID 19 za Kiingereza katika Kiswahili.

Data ya makala haya inaonesha kuwa mabadiliko ya uchopekaji yamefanyika kwa asilimia kubwa zaidi ikilinganishwa na mabadiliko mengine. Kutokana na kukithiri kwa matumizi ya aina hii ya mabadiliko ya kifonolojia, mtafiti amehoji na kutoa hitimisho kuwa hali hiyo inasababishwa na ukweli kuwa mifumo ya lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili hutofautiana. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili hairuhusu mfuatano wa konsonanti kutamkwa kwa pamoja kama silabi moja isipokuwa kwa istilahi zenye konsonanti iliyofuatana na nazali au king'ong'o kama vile /m/, /ɲ/, /ɳ/ na /n/ ilhali lugha ya Kiingereza inaruhusu. Ili kujenga muwala kati ya istilahi zilizotoholewa, data inaonesha kuwa baadhi ya sauti (konsonanti) hudondoshwa.

Suala la utohozi wa istilahi za COVIDI 19 linadhihirisha wazi kuwa istilahi zinazoruhusu mfuatano wa konsonanti mbili (hasa mfuatano usio wa konsonati ya nazali na isiyo nazali) na zaidi kutamkwa kama silabi moja katika lugha ya Kiswahili ni zile zilizotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza. Halikadhalika, udondoshaji hufanyika kwa lengo la kuzifanya istilahi hizo zitamkike kwa kufuata kanuni na taratibu za lugha ya Kiswahili. Mabadiliko mengine yaliyoshughulikiwa ni ya uchopekaji. Kutokana na data ya makala haya imebainika kuwa mchakato huu unahusisha uingizaji wa vipashio katika istilahi za Kiingereza ili istilahi hizo ziweze kukubalika katika mfumo wa lugha ya Kiswahili.

Imebainika pia kuwa kwa asilimia kubwa, istilahi za COVIDI 19 za Kiingereza zimetoholewa katika Kiswahili kwa kuchopeka irabu ya juu mbele /i/. Mabadiliko

haya ya kifonolojia yamechangia katika kupunguza mkururo wa konsonanti katika istilahi za Kiingereza zinazotoholewa katika Kiswahili. Halikadhalika, usahilishaji wa irabu unganifu (dipthong) kuwa irabu sahili (monothong) ni miongoni mwa mabadiliko ya kifonolojia yaliyojitokeza katika makala haya. Katika mchakato huu irabu unganifu za Kiingereza zimesahilishwa kutokana na sababu kuwa mfumo wa lugha ya Kiswahili hauna utaratibu wa irabu unganifu. Jambo hili huwalazimu wazungumzaji wa Kiswahili kusahilisha irabu unganifu ili kupata irabu sahili.

**Marejeleo**

Adika, O. (2013). 'Utohozi wa Maneno-mkopo katika Lugha ya Kijaluo kutoka Kiswahili: Mtazamo wa Mlingano Chanzi'. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Adolph, E. (2014). 'Utohozi wa Istilahi za Kiingereza katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Istilahi za Tiba na Kompyuta'. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Adolph, E. (2019). 'Utohozi wa Nomino za Kiswahili na Athari yake katika Ngeli za Kihaya'. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chomsky, N. Na Morris Halle. (1968). *Sound Pattern of English*. New York: Harper and Row.

Eliah, M. (2012). 'Uainishaji wa Ngeli za Nomino katika Lugha ya Kinyakyusa Kimofolojia na Kisemantiki'. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Fromkin, V. R. Rodman & N. Hyams, (2003). *An Introduction to Language*, (Toleo la 9). New York: Academic Press.

Habibu, M. (2013). 'Mabadiliko ya Kifonolojia katika Lugha ya Kiw'oso'. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. na wenzie, (2007). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu* (FOKISA) Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (2003). *Rearch Methods*: *Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press Kenya.

Mweri, J. G. (2010). *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Njogu, K. (2006). *Sarufi ya Kiswahili Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.

Shembilu, M. (2010). 'Mabadiliko ya Kifonolojia na Kimofolojia wakati wa Utohozi wa Maneno ya Kiarabu katika Kiswahili: Mifano kutoka Kamusi ya Kiswahili Sanifu', katika *Kiswahili*: Juzuu 73.